# JE, UNAO NAFSI ISIYOWEZA KUFA?

**Je, ni kweli kwamba sisi wanadamu huenda mbinguni au kuzimu tunapokufa? Wengi husema ndio! Imani hii inao msingi katika dhana ya moto unaoendelea kuwaka wa kuzimu kama adhabu kwa waovu, na mbinguni kama karama kwa waliokombolewa. Lakini fundisho hili ni la kweli? Je, lilitoka katika Biblia?**

Je, unao *nafsi?* Wewe ni *nafsi?* Je, kunao kitu kukuhusu *kisichokufa* – ambayo haitaweza *kufa kamwe?* Kama ni hivyo, ni lini, na "nafsi" hiyo ilikuja kwa njia gani mwilini mwako? Iliwekwa kwako ulipozaliwa? Ulikuja katika mwili wako wakati mwingine ulipokuwa kama kiinitete? Ulipewa nafsi punde tu ulipopumua, mda mchache baada ya kuzaliwa?

Ikiwa unao nafsi, unaweza kuiguza, kuionja, kuihisi, kuisikia, au kuinusa? Unaweza kuitoa nje na kuitazama? Unaweza kuona nafsi ya wengine? Je, wewe kwa undani wako wote, mawazo za kibinafsi, mazoea, dhana na ndoto, mambo ya siri, mashaka, imani, na hisia, utaweza KUISHI katika mwili huu wa kibinadamu na wa nyama *hata milele?*

Kulingana na mafundisho ya nafsi usioweza kufa, MTU kwa kweli anaishi *ndani ya* mwili usio wa milele. Mwili unaonekana kama nguo usio wa milele. Mtu mwenyewe anakaa ndani ya hiyo nguo usio wa milele; na wakati wa kifo, nguo huo (mwili) hutupwa, huzikwa au kuchomwa, wakati mtu mwenyewe huenda aidha mbinguni, au katika moto wa kuzimu usiozimika! Tamaduni ya Kikatoliki hufundisha kwamba kunazo sehemu tofauti zinazoitwa utakaso.

Unawezaje KUJUA, kwa njia moja au nyingine? *Mamlaka* yako ya mwisho ni ipi wa kuwa na uamuzi wa *kweli* juu ya somo lolote inayohusisha maisha na kifo, hukumu na baadaye?

Ikiwa "mamlaka" ya imani *yako* ni hadithi za maono juu ya kifo, mawasiliano na "nafsi zilizokufa," Taamuli za kisasa, dini za mazoea, au zinazoeleweka kwa wachache, basi usiendelee kusoma zaidi. Nakala hii inakubali BIBLIA, neno lililoandikwa la Mungu kama ilivyo katika maandishi zake za kale (na katika lugha zake za kiasili), kama mamlaka ya mwisho kuhusu somo la kutokufa kwa nafsi.

Mbona wanadamu wengi *wanajishawishi kikamilifu* kuwa wanao nafsi zisizoweza kufa wakati neno nafsi "isiyoweza kufa" HAIPATIKANI popote katika maandiko?

## Mwanadamu ni nini?

Bila shaka, swali kuhusu ikiwa unao nafsi usioweza kufa ndilo swali halisi, Wewe ni nani?

Kwa wasiomwamini Mungu na wanaoamini nadharia ya mageuzi, mwanadamu ni kama nyani asiye na manyoya. Wanaomkana Mungu wanamtazama mwanadamu kama matokeo ya mwisho

wa uwezekano usioonekana; matokea ya mwisho wa milenia usio wa hakika; uchaguzi wa kiasili na kuishi kwa usawa. Bila shaka, wale wanaoikana neno la Mungu wanao IMANI potofu katika nadharia ya baba za mageuzi, na hakuna kisicho kisayansi kuliko nadharia ya mageuzi!

Wale wanaoamini katika Uumbaji – wanaojua na kuelewa kwamba maisha unaweza kutoka tu kwa maisha yaliyopo wa *aina sawa*; wanaoelewa kuwa sheria inaweza kutoka tu kwa Mpaji wa sheria mkuu; ukamilifu huo, usawa, utegemeano, na *muundo* wa ajabu unaweza kutoka tu kwa MBUNI MKUU – ifahamu vizuri.

Wanajua kwamba familia ya kibinadamu ilianza na mwanadamu mmoja, na kwamba mke, aliyeumbwa kimiujiza kutoka kwa mwili wake kama kiumbe cha kipekee na wa kiasili kama Adamu mwenyewe walianzilisha *familia ya kwanza*.

Katika tukio lolote, hata kama ni kwa ajili ya mahojiano pekee, wale wanaodai kuwa katika dini ya Kikristo na wanaamini katika uvuvio wa Biblia lazima waweze kueleza “Mwanadamu ni nini?” kutoka kwa mtazamo wa akaunti ya Uumbaji ilivyofunuliwa katika Biblia.

Mungu alipomwumba mzazi wetu wa kwanza Alisema, “Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi; ambayo katika hiyo ulitwaliwa; KWA MAANA U MAVUMBI WEWE, nawe mavumbini utarudi” (Mwanzo 3:19).

Mungu alikuwa akizungumza na Adamu. Alikuwa akiwasiliana na *mwanadamu mwenye ufahamu!* Hakumwambia Adamu kwamba *mwili* wake tu uliundwa kwa vipengele vya ardhi, na kwamba Adamu alikuwa kwa hakika moyo uliofungwa katika mwili wa muda mfupi ulioonekana! Hapana! Alisema Adamu alikuwa udongo mwekundu au matope mwekundu – kwa kuwa hiyo ndiyo maana haswa wa neno la Kiebrania “mavumbi.”

Tazama! “Bwana Mungu akamfanya mtu kwa *mavumbi ya ardhi,* akampulizia puani *pumzi ya uhai;* mtu AKAWA nafsi hai.” (Mwanzo 2:7).

Kumbuka, Biblia haikuandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Mara mingi, Biblia iliandikwa kwa Kigiriki na Kiebrania; Kiebrania ikitumika sana katika Agano la Kale, na Kigiriki ikitumika sana katika Agano Jipya.

Hakukuwa na uwepo wa neno *nafsi (soul)* wakati sawa Biblia ilipoandikwa. Ni neno la Kiingereza, lililo karibu kwa kipekee kupitia kielelezo la *kikanisa.*

Kwa kweli, kama utakavyoona, neno la Kiingereza (soul) au *nafsi* unapaswa kufutwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza, na *kubadilishwa* na maneno mengi yanayowezekana na kukaribiana kwa kielelezo ya neno la Kiebrania *nephesh.*

Kwa kuwa neno la Kiebrania *nephesh* ndicho kinachotafsiriwa *nafsi (soul)* kwa Kiingereza!

Kwa kiasili basi, utafutaji wetu wa maarifa na kuelewa unashugulikia neno la Kiebrania *nephesh!*

Ni nini maana ya neno la Kiebrania *nephesh?*

*Exhaustive Concordance ya Strong* inasema: "(5315) *nephesh* ni; kiumbe kinachopumua, k.v mnyama au nguvu: ikitumika sana sana kwa uhalisi, kwa mfano (wa kimwili au kiakili); hamu, mnyama, mwili, pumzi, kiumbe, kufa, matamanio, kuridhika, samaki, mzuka, mchoyo, yeye, moyo, (hatari ya maisha; kuwa katika hatari), tamaa, mwanadamu, mimi, akili, mauti, mmoja, ubinafsi, mtu, raha, (yeye, yangu, yako) ubinafsi, wao (yao), kuua, nafsi, kidonge, wao, kitu, mapenzi, itakuwa nayo."

*Orodha ndefu sana!* Unaona, neno la Kiebrania *nephesh* unahusisha "uwepo"! Vivyo, unao matumizi mingi, juu ya kimwili, mnyama, MAISHA *inayopumua* ya viumbe vya nyama na damu! Tazama kwamba inaweza kutafsiriwa "kufa," au hata "mnyama" au "kiumbe" na vile vile "tamaa," "mauti" au "mtu."

Je, ulijua kwamba neno la Kiebrania *nephesh* inatumiwa mara mingi kwa aina za maisha ya kichini KABLA ya kutumiwa kuhusu mwanadamu katika Biblia!

Tazama Mwanzo 1:20 ambapo *nephesh* hutumiwa kama, "kitu kiendacho cha uhai"; katika aya ya 21 "kiumbe cha uhai"; aya ya 24 "kiumbe hai," na "mnyama"; aya ya 25 "mnyama" (ikirejelea nyangumi, samaki wa baharini, na maisha ya chini yaliyo baharini)!

Katika picha hii ya maelezo ya uumbaji wa wanyama wote na wa baharini, neno *nephesh* hutumiwa mara kwa mara!

Sasa soma Hesabu 19:11: "Mtu agusaye *maiti* yeyote atakuwa najisi muda wa siku saba." Katika andiko hili, sheria za kutakaswa chini ya Walawi zinajadiliwa. Mtu atachukuliwa kuwa najisi ikiwa amegusa maiti uliyooza au mwili wa mnyama au mwanadamu.

Tusome aya ya 22, "Na kitu chochote atakachokigusa mtu aliye najisi kitakuwa najisi; na mtu (nafsi) [*nephesh*] atakayekigusa kitu hicho atakuwa najisi hata jioni."

Neno sawa lililorejelewa nafsi katika aya ya 22 (inayopaswa kutafsiriwa "mmoja" au "mtu") imerejelewa kama "maiti" katika aya ya 11! Iweke akilini mwako na ikae humo wakati wote. Neno sawa inayotafsiriwa "nafsi" kwa uhalisi katika sehemu kadhaa kwenye Agano la kale hutafsiriwa hapa kama "maiti."

Sasa soma Ezekieli 18:4, 20: Tazama, roho [*nephesh*] zote ni mali yangu; kama vile roho [*nephesh*] ya baba ni mali yangu, ndivyo ilivyo roho [*nephesh*] wa mwana mali yangu, roho [nephesh] ile itendayo dhambi ndiyo itakayokufa ["nafsi" hiyo au *nephesh*]." Hapa, hii ingerejelewa wazi kwa Kiingereza kama, "Tazama, watu wote ni wangu; kama vile mtu wa baba, ndivyo ilivyo mtu wa mwana, mtu atendaye dhambi ndiye atakayekufa"!

Mkazo wa Maandiko ni *jukumu la kibinafsi* mbele ya Mungu! Kile Mungu anasema kupitia nabii Ezekieli ni kwamba hakuna atakayetoa visababu kwa dhambi na kwamba hatuwezi "kuwalaumu" wengine kwa dhambi tulizozitenda sisi *wenyewe*!

Andiko hili *halijatolewa* kama somo ikiwa nafsi haziwezi au zinaweza kufa; hata hivyo, kwa kuwa maandiko inasema wazi kwamba "roho ile itendayo dhambi ndiyo ITAKAYOKUFA," inawakilisha hitimisho la uthibitisho wenye nguvu kwamba neno la Kiebrania wa "nafsi" au *nephesh* unamaanisha *kimwili, unaokufa, maisha ya muda mfupi,* na *haina chochote kamwe* kuhusu kutokufa.

Sasa jiulize, "Biblia inasema kwamba nafsi inaweza kufa kulingana na maana yake ya neno hilo?"

Jibu lako bila shaka ni "NDIO!"

Basi, kwa mtazamo wako, unaona *uthibitisho* kamili kwamba neno lililotafsiriwa kwa Kiingereza (soul) au nafsi *haina chochote* kamwe kuhusu kutokufa au mambo ya kiroho; lakini inahusu mambo ya kimwili na uwepo wa wanadamu na wanyama wa damu na nyama!

Neno *nephesh* inapatikana katika vifungu 243, na inatafsiriwa kwa njia kumi na moja. Tazama kwamba maelezo "wafu" inatafsiriwa moja kwa moja kutoka kwa neno la Kiebrania *nephesh* katika vifungu vifuatavyo: Mambo ya Walawi, 19:28; 21:1; 22:4; Hesabu 5:2; 6:11.

Neno sawa linalotafsiriwa "nafsi" mara mingi hurejelewa kama "maiti" katika Hesabu 9:6, 7, 10.

Inatafsiriwa kama mwili katika Mambo ya Walawi 21:11; Hesabu 6:6; 19:11, 13; na pia katika Hagai 2:13.

## Vipi Kuhusu Agano Jipya?

Neno la Kigiriki *psuche* ndilo neno pekee linalotafsiriwa "nafsi" katika Agano Jipya. Utapata neno hilo mara 105 katika Agano Jipya, ambapo inatafsiriwa mara hamsini na nane tu, lakina pia huweza kurejelewa kama kama "maisha" mara arobaini, "akili" mara tatu, na "moyo," "kwa moyo," "sisi," na "wewe" mara moja kwa kila moja.

Neno la Kigiriki *psuche* ni neno sawa na neno la Kiebrania *nephesh* na hutumika kwa njia sawa kote katika Agano jipya.

Kwa mfano, *psuche* inatumiwa kwa wanyama wa chini, kama vile umeona *nephesh* ikitumika kwa aina za maisha ya chini katika sura ya kwanza ya kitabu cha Kutoka! Katika Ufunuo 8:9 neno la Kigiriki *psuche* (kumbuka hili ndilo neno tu katika Kiingereza liliotumiwa kurejelea neno nafsi), inarejelewa kama "maisha." Tazama pia Ufunuo 16:3, ambapo maisha ya kichini yanazungumziwa, walakini neno "nafsi" inatumika. Soma andiko la mwisho kwa makini! Inaelezea mapigo yatakayokuja juu ya nchi na bahari, na inasema, "vitu vyote vyenye roho ya

uhai katika bahari VIKAFA"! Hapa kunao dhibitisho kimoja tena kutoka kwenye Agano Jipya kwamba neno nafsi kama ilivyopata njia yake katika lugha ya *Kiingereza* humanisha *kiumbe*, au *kitu chochote chenye uhai* kinchoweza kufa! Katika kesi hii inatumika kwa aina mbali mbali ya maisha (ambapo kunazo *maelfu*) katika bahari!

Mara mingi, rubani wanaowasiliana kwa mpango wa ndege husema wanao nafsi wengi kwenye bodi wakitumia neno hilo na kuibadilisha kama watu. Wakati kichwa ya gazeti huzungumzia "nafsi" wengi sana waliokufa kwenye meli iliyozama, inatumia neno hilo kwa njia sawa inavyotokea katika Biblia mara kumi na minne tofauti! Kwa udhibitisho, soma Matendo 2:41-43; 3:23; 7:14; 27:37; Warumi 2:9; 13:11; 1 Wakorintho 15:45; Yakobo 5:20; 1 Petro 3:20; 2 Petro 2:14; Ufunuo 6:9; 18:13; 20:4.

Katika vifungu hivo, neno la kigiriki *psuche* hutumika kwa *maisha ya mwanadamu*, ambayo huweza kuharibiwa au kupotea.

Hoja ni, neno hilo la Kigiriki huweza kutumiwa mara mingi kama neno la Kiebrania *nephesh* na pia huweza kutumiwa kwa hisia za mwanadamu! Kwa mfano, *psuche* hutafsiriwa kama yafuatavyo: "akili," "sisi," "wewe," "moyo," na "kwa moyo wote."

Neno la Kiingereza *nafsi* katika Agano la Kale karibu *mara zote* huchukuliwa kutoka kwa neno la Kiebrania *nephesh* na HAIMAANISHI chochote kisichoweza kufa; kama vile tu neno la Kiingereza nafsi katika Agano Jipya hutoka kwa neno la Kigiriki *psuche*, na haina maana ya kutoweza kufa.

## Nini Hutokea wakati wa Kifo?

Ni wazi kutoka kwa lugha za kiasili za Biblia (Kiebrania na Kigiriki) kwamba mwanadamu hufa kwa njia sawa kama mnyama. "Kwa maana linalowatukia wanadamu linawatukia wanyama; jambo moja lawatukia; anavyokufa huyu *ndivyo anavyokufa huyu;* naam, wote wanayo pumzi moja; wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama; kwa maana yote ni ubatili. Wote *huendea mahali pamoja;* wote hutoka *katika mavumbi;* na hata *mavumbini hurudi* tena." (Mhubiri 3:19, 20).

Tazama jinsi waandishi wa Biblia walioongozwa *walielezea* hali ya kifo: Ayubu aliandika, "Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa taabu. Yeye huchanua kama vile ua, kisha hukatwa; hukimbia kama kivuli wala hakai kamwe" (Ayubu 14:1, 2).

Mungu alimwongoza Daudi kuandika sana kuhusu somo la maisha na kifo. Daudi alisema, "Lakini mwanadamu hadumu katika heshima, bali amefanana na *wanyama* wapoteao. Kama *kondoo* wamewekwa kwenda kuzimu [*sheol*], na mauti itawachunga; watu wanyofu watawamiliki asubuhi; umbo lao litachakaa, kao lao ni kuzimu [*sheol*]. Bali Mungu atanikomboa nafsi [Kiebrania, *nephesh* – inayomaanisha MAISHA] yangu, atanitoa *mkononi mwa kuzimu* [Tazama kuzimu unao NGUVU juu ya aina ya "maisha" inavyoelezewa na neno la Kiebrania

*nephesh*]: Maana atanikaribisha. Mwanadamu mwenye heshima, iwapo hana akili, amefanana na wanyama wapoteao." (Zaburi 49:12-20).

Kwa sababu Mungu mwenye Nguvu anatufunua sisi wanadamu – viumbe vya mikono Yake – sisi tu *wana* Wake na kwamba *tutafufuliwa* KUTOKA KWA KIFO (Luka 20:36), Alimwongoza Daudi kuandika, "Ina thamani machoni pa Bwana mauti ya wacha Mungu wake." (Zaburi 116:15).

Kuna mifano mengi katika Biblia kuhusu kinachotokea wakati wa kifo!

HAKUNA popote katika Biblia ambapo neno "nafsi isiyoweza kufa" hupatikana! Kunao "roho katika mwanadamu," iliyotajwa katika Biblia, ambayo ni somo la kina. Kwa ufupi, roho katika mwanadamu ni ile *kiini cha kiroho* inayoinua akili ya mwanadamu katika kiwango iliyo juu ya akili dogo ya wanyama. Hii inatajwa na Ayubu na Mtume Paulo waliosema jinsi Roho Mtakatifu wa Mungu "hushuhudia na roho yetu" kwamba sisi tu wana wa Mungu.

Biblia hufunua wazi kwamba Mungu huzalisha WATOTO!

Kama vile wanadamu hawazalishwi bila ya maisha kuzalisha maisha (maisha ya kiume ikijiunga na ya kike), hivyo Mungu mwenye nguvu anafunua kwamba Roho Wake Mtakatifu haiungani na *mwili* tu; lakini kwamba kuna roho katika mwanadamu ambayo katika hiyo nguvu yetu ya mapenzi, kujitolea kwetu, uwezo wa kufanya maamuzi na *utu* wetu huwa!

Biblia inaposema kwa mifano juu ya "moyo," inasema juu ya sehemu ya akili ya mwandamu ambapo MITAZAMO yetu na MIENENDO yetu huwa. Ujuzi wa hivi karibumi wa kisayansi unafunua kwamba akili ya mwanadamu unao sehemu mingi tofauti. Sehemu zingine za kiakili zinadhibiti vitu vile kama uratibu wetu, usawa, uwezo wetu wa kifizikia na riadha; sehemu zingine hushughulikia mitazamao wa hisia kama vile mfumo mkuu wa neva, macho na kadhalika. Sehemu zingine hushughulikia kumbukumbu, na mbele na nyuma ya kichwa inayodhibiti mawazo ya mwanadamu ambayo ni sehemu ya KUFANYA UAMUZI ya kiakili.

Pengine kuna maana zaidi kwa wale wanaopokea "alama ya mnyama" kwenye *vichwa vyao* (kumaanisha kwa *mapenzi*; kwa ruhusa yao, makubaliano na uchaguzi) wakati mmoja anapoelewa ukweli huu rahisi!

Lakini hii roho katika mwanadamu sio ile isiyoweza kufa! Neno la Mungu linasema wazi kwamba Mungu tu hawezi kupatwa na mauti (1 Timotheo 6:16)! Mwanadamu *anafunuliwa* kama yule aliye na uwepo wa muda mfupi, wa kimwili, wa kifizikia – *wa mavumbi!* Anasemekana kuwa wa kupotea na kuoza. Walakini, ifikirie kwa undani kwa muda mfupi. Jifikirie kama muundo mdogo zaidi wa maisha kutoka kwa baba yako alipoendana na mama yako. Muundo iliyopaswa kutoa umbo lako la kimsingi, urefu, sura, rangi ya macho na manyowa, mchoro wa ngozi, talanta, na uwezo yalikuwemo katika darubini ndogo ya maisha. Mungu mwenye Nguvu anajenga katika maisha yetu ya Kikristo muundo kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu inayoweza kuzalisha kiumbe "kipya katika Kristo" unaojiwasilisha na *roho ya mwanadamu!*

Hata wakati baba yako wa kibinadamu alikutia muhuri kwa utambulisho wake – alikupatia JINA – kwa hivyo Baba wetu aliye mbinguni anatia muhuri Wake mwenyewe, jina Lake, na utu Wake kwa wana Wake!

*Mafundusho ya uongo* juu ya kutokufa kwa nafsi *unaficha ukweli huu mkubwa!*

Ikiwa Mungu anakuwezesha kuelewa ukweli za kindani wa Neno Lake kupitia nakala hii, basi apongezwe Mungu mwenye Nguvu! Ikiwa Mungu anafunua ukweli za kindani kwako, unapaswa kuenda katika kitabu cha Warumi 8 kisha usome kwa kuelewa vizuri sura mzima. Sana sana unaposoma sura hii muhimu, soma aya ya 29! "Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye [Yesu Kristo] awe MZALIWA WA KWANZA miongoni mwa NDUGU WENGI"! Ndio, hata vile Yesu Kristo alivyokuwa mzaliwa wa kwanza kwa wanadamu, yeye pia alikuwa MZALIWA wa kwanza kutoka kwa wafu! Ni wazi! Ni rahisi!

Kipengele kikubwa tunayoona ni ile ya MAISHA! Tunaona kipengele cha *miujiza* kwamba maisha hutokea kwa maisha ya hapo awali wa aina sawa; kwamba maisha hujiendeleza kimsingi; kwamba yanayofanana yanajizalisha yenyewe, aina kimoja huzalisha aina hiyo kimoja, na kwamba sisi wanadamu, kupitia upendo katika ndoa, tunazalisha *aina yetu wenyewe!*

Mungu mwenye nguvu huzalisha *aina Yake!*

Huu ni UKWELI mkubwa mno!

Kama bado unadadisi kuhusu yale umejifunza ukisoma nakala hii, tunakusihi utuandikie kwa fasihi zaidi.

Kanisa la Mungu la Kimataifa linakuhimiza *kusoma* Neno la Mungu.